



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA  
THE HANSARD**

Tuesday, 6<sup>th</sup> May, 2025

Third Assembly – Fourth Session  
TWENTY FIRST SITTING

*[The County Assembly met at 12:10p.m at the County Assembly Buildings]  
[The Temporary Speaker (Hon. Frankline Makanga) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Let us take our seats. Yes, Clerk?

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

**VISITORS FROM THE MOMBASA COUNTY YOUTH LEADERS' ASSOCIATION**

Honourable Members, we are honoured to have visitors from the Mombasa County Youth Leaders Association. I take this earliest opportunity to welcome you all to this Honourable House; this is the legislative Assembly for the County Government of Mombasa as established by the Constitution of Kenya, 2010. We have the following in our public gallery:

1. Aunt Goldsray - President,
2. Mgeni Juma - Deputy President,
3. Farhiya Juma - Deputy Secretary General,
4. Cynthia Juma - Personal Assistant to the President,
5. Milton Sami - Speaker of the Assembly,
6. Patrick Gathogo - Clerk,
7. Ahlam Ahmed - Deputy Clerk,
8. Eunice Kalewa - Deputy Speaker,
9. Saumu Abdallah - CS Environment,
10. Nassim Mohammed - CS Blue Economy,
11. Gaylord Luangwu - CS Partnership,
12. Michael Nabwana - Representative Nyali,
13. Mary Mativo - Miritini Ward Representative,
14. Nashli Ibrahim - Representative for Tononoka Ward,
15. Mwanaharusi Juma - Representative for Ganjoni-Shimanzi,
16. Eliud Okabi - Kongowea Ward,
17. Patrick Nyakundi - Tudor Ward,
18. Tabitha Joy - YMCA,

19. Dyuke Mogaka - Shanzu Ward,
20. James Katana - YMCA,
21. Mary Kamau – YMCA,
22. Muhammad Twalib - Advisory Board Member.

*[Applause]*

So, I take this opportunity to welcome you all to Assembly. I hope you will have a learning session. Thank you. Yes, Clerk?

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri, Leader of Majority Party, please lay the Paper? That is the Mombasa County Program Based Budget Estimates for the Fiscal Year, 2025/2026.

### PAPER

THE MOMBASA COUNTY PROGRAM BASED BUDGET ESTIMATES FISCAL YEAR 2025/2026

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I rise to lay Paper the Mombasa County Program Based Budget Estimates, Financial Year, 2025/2026.

*[Paper laid by Honourable Mwamwiri on behalf of Honourable Kibwana Swaleh]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you. Honourable Members, the Mombasa County Programme-Based Budget Estimates Fiscal Year 2025/2026 laid today stands committed to the Committee on Finance, Budget and Appropriations for consideration. Yes, Clerk?

### NOTICE OF MOTION

BUDGETARY ALLOCATION FOR ROAD MAINTENANCE MACHINERY TO ENHANCE SERVICE DELIVERY

Yes, Honourable Allen Katana, please give the notice?

*[Hon. Katana gives the Notice of Motion on behalf of Hon. Jacktone Madialo]*

**Hon. Katana:** Thank you, Honourable Speaker. I beg a Notice of Motion on Budgetary Allocation for Road Maintenance Machinery to Enhance Service Delivery. Mr. Speaker Sir, I beg to give a Notice of the following Motion;

*AWARE THAT under the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010, the function of the County government includes County Transport, maintenance of road and provision of public works and related services.*

Mr. Speaker,

*FURTHER AWARE THAT effective service delivery in the infrastructure sector depends heavily on the availability and use of specialized equipment such as graders, backhoes and lorries for activities including road maintenance, drainage, cleaning, clearing, waste removal and emergency response.*

*COGNIZANT THAT the Department of Transport and Infrastructure in the County of Mombasa is currently operating with inadequate mechanical support due to the lack of critical machinery, specifically a grader, a backhoe and lorries, thereby severely constraining the ability to deliver essential services in timely, efficient and cost-effective manner.*

Mr. Speaker,

*CONCERNED THAT this shortfall has led to delay in road repairs, poor drainage management and reliance on hired equipment with results in higher costs to the County and compromised services standards to the residents.*

Mr. Speaker,

*NOTING THAT the County is in the process of preparing its budget for the upcoming financial year and the proper planning at this stage presents a timely opportunity to address the existing machinery gap.*

I, therefore urge this Assembly, Mr. Speaker,

- 1. To resolve that the Department of Transport and Infrastructure to prioritize and include the budget estimate for the financial year adequate funding for the procurement of one grader and backhoe and two lorries. Ensure that once procured, the machinery is strategically deployed across the sub-counties for equitable and efficient use.*

Mr. Speaker,

- 2. To develop a clear maintenance and operation plan for the equipment to ensure long-term utility and accountability.*

Lastly,

- 3. To engage relevant stakeholders, including the County treasury, to secure the required budget allocation without delay.*

I, thank you, Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Allen. Yes, Clerk? Yes, Honourable Allen Katana, please proceed to move the Motion?

### **MOTION**

BUDGETARY ALLOCATION FOR ROAD MAINTENANCE MACHINERY TO ENHANCE SERVICE DELIVERY

*[Hon. Katana moved the Motion on behalf of Hon. Madialo]*

**Hon. Katana:** Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

*AWARE THAT under the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010, the functions of the County governments include County Transport maintenance of roads and provision of public works and related services*

*FURTHER AWARE THAT effective service delivery in the infrastructure sector depends heavily on the availability and use of specialized equipment such as graders, backhoe and lorries for activities including road maintenance, drainage clearing, waste removal and emergency response*

*COGNIZANT THAT the Department of Transport and Infrastructure in the County government is currently operating with inadequate mechanical support due to the lack of critical machinery, specifically a grader, a backhoe and lorries thereby severely constraining their ability to deliver essential service in timely, efficient and in costly effective manner*

Mr. Speaker,

*CONCERNED THAT this shortfall has led to delays in road repairs, poor drainage management and reliance on hired equipment which results in higher cost to the County and compromised service standard to the residents;*

*NOTING THAT the County is in the process of preparing its budget for the upcoming financial year and that proper planning at this stage presents a timely opportunity to address the existing machinery gap;*

I, therefore ask this Honourable Assembly, Mr. Speaker to RESOLVE that;

- 1. The Department of Transport and Infrastructure to prioritize and include in the budget estimates for the forthcoming financial year adequate funding for the procurement of one grader and a backhoe and two lorries to ensure that once our procedure, the machinery is strategically deployed across the sub-counties for equitable and efficient use,*
- 2. Develop a clear maintenance and operation plan for the equipment to ensure long-term utility and accountability;*

Lastly, Mr. Speaker,

- 3. To engage relevant stakeholders including the county treasurer to secure the required budgetary allocation without delay.*

With this Honourable Speaker, I humbly ask the very senior Honourable Member Honourable Maimuna to second. Thank you.

**Hon. Maimuna Salim:** Thank you, Mr. Speaker. Thank you, the Mover of the Motion. I stand to second the Motion.

*[Applause]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Allen and Honourable Maimuna. Honourable Members, I now propose the question that the Motion moved by Honourable Allen Katana on behalf of Honourable Jacktone Madialo be debated in this House.

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Allen Katana?

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni wakaribishe wageni ambao tuko nao hapa. Pili, niliweke wazi ya kwamba mjadala huu wa leo Mheshimiwa Spika kama ulivyotangulia kusema kwa hekima yako si wangu ni wa Mheshimiwa Jacktone Madialo wa Mikindani na mimi, nimejitolea kuusimamia na kuusimamisha kwa sababu najua hekima ya viongozi hawa wataupitisha. Uoga wangu nimesikia sauti ya ibilisi lakini Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Allen, I doubt if we have a Member in this House by the name *ibilisi*.

**Hon. Katana:** I withdraw.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yeah, and apologize.

**Hon. Katana:** I withdraw and apologize.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you.

**Hon. Katana:** Thank you, Mr. Speaker. Mheshimiwa Spika kwa kila Mheshimiwa Spika aliyekaa mahali hapa na yuko nyanjani kikweli atajua shida watu wetu wanazopitia na barabara zao. Mheshimiwa Spika mkononi mwangu nina rununu kwa hivi sasa kwa mtandao wangu wa *WhatsApp* Mheshimiwa Spika umejaa picha nyingi za mateso, watu wetu barabara zao hazipitiki, majumba yao hayalaliki kwa sababu Mombasa Kaunti imekuwa na upungufu wa Vyombo vya kufanyia kazi. Mheshimiwa Spika iende kwa kumbukumbu ya Jumba hili ya kwamba imejulikana sana kwa muda mrefu Mombasa cement amekuwa akitusaidia kama umma kwa mambo ya matibabu, kwa mambo ya vyakula na mengi mengineyo lakini kwa muda mrefu Bamburi Portland Cement imekuwa haisaidii lakini kwa mara ya kwanza. Mimi mwenyewe nimeenda pale nikapiga nduru ni kalinganisha utenda kazi wa Mombasa Cement nao wakaona uhitaji pia wao wanastahili kupeana kwa jamii.

Mheshimiwa Spika hivi sasa ninavyo kwambia ukinipa ruhusa nitaingia kwa gari yangu nitakuletea barua nimepewa lori mia mbili za saruji za Bamburi Portland Cement lakini wameniambia hatutakupi saruji na tukupe na usafiri, wewe mwenyewe tafuta usafiri usafirisha saruji ukaitandaze popote ndani ya Wadi ya Shanzu kama unavyotaka. Nimechukua miezi mitatu Mheshimiwa Spika kuomba department ya usafiri inipe angaa lori moja. Nimeonyeshwa malori mengi pale kwa Yard pale fire station, nimeonyeshwa malori mengi pale kwa yadi pale kwa *inspectorate*, nimeenda mpaka kwa karakana za watu binafsi kuna magari ya Kaunti yamelala pale mabovu na kwa sababu ya hiyo Mheshimiwa Spika nataka nikutajie kijiji ambacho kinaniuma sana, nimembeba mpaka Waziri wa Kaunti akalalamika yeye mwenyewe tuko na *grader* moja ambayo ni mbovu na bado hata ukipewa *murram* kuna mashini nyengine ambayo ni lazima itumike ili ihakikishe kumetandazwa vilivyo Mheshimiwa Spika, Waziri naye akaniambia hiyo nayo ni moja na ni mbovu.

Kwa bahati mbaya kila ninapoulizia naambiwa imeharibika Mwakirunge lakini nalielewa kwa sababu Waziri wa Mazingira ni Naibu wa Gavana sasa inabidi iende huko ikasawazishe pale Mwakirunge panapo tupwa takataka. Mheshimiwa Spika itakuwa kuna Mheshimiwa ambaye ana matatizo ya akili atakayepinga Mswada huu na ndio maana kwa hekima uliyonipa Mheshimiwa Spika nikachagua ni nani Mwenye hekima ya kuanza kuunga Mswada huu akawa ni Mheshimiwa ambaye ana uzoefu ndani ya Bunge hili naye ni Mheshimiwa Maimuna. Mheshimiwa Spika ninachokiomba Waheshimiwa wenza tunajua *Standing Order* 204 inasema sisi hatuna uwezo wa kutoa vitu kama hivi na kusema tunataka vifanyika lakini sisi hapa hatusemi watumie pesa kwa muujibu wa hii maombi ya Mheshimiwa madialo ni kwamba tunaikumbusha *Executive Arm* ya kwamba wanapopanga mambo yao wahakikisha wamepangilia

vitu hivi muhimu. Kwa hayo machache Mheshimiwa Spika nangoja yule ambaye ana akili kidogo ya matatizo, akaupinge Mswada huu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Allen Katana. However, for the records is that all the Honourable Members of this House are sane, they are of sound mind and that is why they were elected to represent the people of Mombasa. Yes, Honourable Prischillah Mumba Majority Whip...

*[Applause]*

Please make your contribution.

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kutupa afya na kukutana katika Jumba hili na pia tunamshukuru Mwenyezi Mungu huyu huyu kwa kutupa nyakati za mvua, nyakati za kuleta neema lakini pia huwa ni ngumu kwa upeo wa mwanaadamu. Tatu ninasimama kuwashukuru waliokuja kutuangukia katika Bunge hili na haswa nikinukuu manake nimesikia jina kutoka Ganjoni...

*[Applause]*

Na ni mama kama mimi na ninamtakia kila la heri hata kijiti nikikitoa hapa nafikiri nitakielekeza kwake moja kwa moja. Nimesimama hapa kuunga Mswada huu mkono mia fil mia, kwanza nikitangaza kuwa mimi ni mmoja wa Kamati ya Barabara na Miundo Misingi na katika Bunge la pili Mheshimiwa Spika, maana nilikuwa hapa mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti wa Barabara na Miundo Misingi na Mheshimiwa Katana amenifurahisha sana aliposema malori ambayo yapo katika Yadi, malori ambayo yako katika *Inspectorate* sasa hivi yamechoka, malori yale wakati nilipokuwa Mwenyekiti wa Barabara na Miundo Misingi ninajivunia kuwa nilipigania mpaka tukaweza kuwa na malori yale wakati wa kipindi cha muhula wa pili na sasa ni wakati muafaka kwa sababu yamefanya kazi mpaka yamefikia kiwango ya kuwa yamechoka na kazi ya Mombasa Kaunti si rahisi, ni kazi kubwa sana na ni wakati muafaka kwa sababu tunaelekea kwa upande wa bajeti na tunaona tusiposukuma hali jambo tutakuwa tumeachwa nyuma na magari yetu yote yamekuwa yamesimama. Pili, kitu nitaweza kusema kuwa pia tunashukuru kwa sababu Mheshimiwa Gavana alikuwa pia amekuwa katika wakati wa kulipa yale masalio yalikuwa yako katika kununua yale magari ikawa pia kuna *delay* kidogo kwa sababu kulikuwa lazima kumaliziwe yale magari yalikuwa yametangulizwa kulipiwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi kitu ningesema ni kweli tuko na shida na ukiangukia katika Mombasa Kaunti yote kwa kila Wadi zote 30 nikiwa nina ushahidi niumewahi kuzitembea wakati nilipokuwa Kiongozi wa Kamati hiyo niliona changamoto...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Allen and Honourable Manuari, Honourable Morgan and Ibrahim Omondi you should be consulting in low tones otherwise you are out of order. Proceed.

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunilinda na hata nashangaa sana kwa sababu ninayezungumza hapa ni Kiranja wa Bunge ambaye mimi ndio nategemewa kutuliza Bunge hili kama *prefect* na leo nazungumza na wengine wanazungumza...

---

[Interruption]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Prischillah, please proceed and make your contribution...

[Interruption]

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika najaribu kujitetea...

[Interruption]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): I have already given direction!

[Interruption]

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Kwa sababu naona kuna hujuma fulani...

[Interruption]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Prischillah, I have already given direction and you are protected, please make your contribution.

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika ninaendelea kujenga Hoja yangu kwa sababu nimeendelea kusema katika Wadi zote 30, tuna matatizo ya barabara, tuna matatizo ya hizi *drainage system* ambazo kila baada ya muda zinakuwa nyengine tutasema ni uchafu ukiingia unajifunga kwa sababu hatuna kitengo maalum katika Kaunti cha mara kwa mara kwenda kuzibua ile mitaro na kuweza kuiweka wazi na kutengeneza zile *drainage system* ziwe ziko wazi ziweze kupitisha maji bila matatizo, sana huwa tunangojea mpaka wakati mvua kama hii ikiwa kali ndio sasa tunaona watu wanakimbia kwenda kuchokora na wakati kama huu Wadi zote zimefurika kwa sababu mvua hainyeshi robo robo, inanyesha kwa pamoja sasa ikiwa Wadi zote 30 kila Wadi ina shida ya hizo *drainage*, ina shida ya barabara kupitika, haina *grader* ya kukwangura ili njia ziweze kuwa tambarare inakuwa tatizo kubwa ndio pale unakuta Mheshimiwa Spika kwa wakati huu sisi kama viongozi tunapitia wakati wa matusi, maana yake inaonekana kama ambaye hatujielewi katika kazi zetu na hali tuna Wizara inayohusika ambayo ina vitengo ambavyo vinavyohusika ambavyo vina vifaa ambavyo hata kama ni kidogo lakini viko vya kuweza kufanya zile kazi ambazo tunaziita *emergency work* ambayo hiyo kazi ingelikuwa ilifanywa kama mwezi mmoja nyuma kwa sababu kipindi cha mvua tunakielewa...

[Interruption]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, Honourable Leader of Majority, are you up on...

[Interruption]

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Mheshimiwa Spika sitaki kujuzwa....

[Interruption]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): *Wait first* huwezi kata kujuzwa kabla hujajua unaambiwa nini?

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ndio nakwambia kwa sababu mimi nimesema...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): For the records of the Assembly let us hear from the Leader of Majority. Why are you standing Leader of Majority?

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Mheshimiwa naomba kujuza Jumba; nina wasiwasi na lugha iliotumika kama ni Kiswahili sanifu ama ni Kiswahili cha vichochoroni maeneo ya Shimanzi Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika inapokuja suala la kusafisha maji taka na kadhalika, ufasaha wake ni kuzibua mitaro sio kuchokora inavyotumika kuchokora Mheshimiwa Spika inatutia wasiwasi hii lugha na hapa tuna wataalam wa kuchokora.

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Mwamwiri labda utueleze kuchokora ni nini, utupe kwa mfano kuchokora ni nini?

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Mheshimiwa kwa heshima niliyo nayo kwa Jumba hili nitaomba nihifadhi ufafanuzi wa neno kuchokora lakini tu nimuombe Mheshimiwa atumie neno kuzibua badala ya kuchokora. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Ahsante Mheshimiwa Mwamwiri nafikiri Mheshimiwa Prischillah (Shillah) umeweza kuelekezwa kwa lugha ya ufasaha unaweza endelea sasa kupeana maoni yako.

**The Majority Party Chief Whip** (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika nimeelewa lakini kama unavyojua katika hali yetu ya kuzungumza kuna lugha nyingi tunatumia bora ieleweke tu nimetamka nini kwa sababu neno nililotamka Mheshimiwa Spika si kuwa tu halieleweki ndio pale nikakwambia sitaki kujuzwa maana nilijua natafutwa vineno vidogo vidogo. Ahsante Mheshimiwa Spika nimekubali kwa kurekebisha huko lakini maneno huwa ni mengi ya kuweza kutiwa katikati ya mdomo, kwa hivyo mimi sitaki kutumia muda mrefu kwa sababu najua kuna wenzangu wanataka kuchangia lakini nimejaribu tu kueleza ile changamoto ambayo tuko nayo ambayo inafanya sisi viongozi inafikia wakati sisi tunatukanwa na wajibu wetu sisi ni kutunga sheria ama kufuatilizia ili tuangalie kwamba je hili limetendeka sasa tunapitisha huu Mswada kwa haraka haraka uje uingie katika bajeti inayokuja mwezi huu wa saba tutakapokuwa tunaipitisha na lau tukikosa kuwa kumewekwa matarajio haya tunayotaka maana yake haya magari yakiwekwa na yakisema yatanunuliwa tutapunguza idadi ya fitina mitaani na tutaona kazi ikiendelea kufanyika. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ninasimama kuunga mkono na nataka huu Mswada upite hata sasa hivi kwa sababu tunahitaji haya *ma grader* na magari yaweze kufanya kazi.

*[Applause]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Prischillah. Yes, Honourable Maimuna Salim please make your contribution?

**Hon. Maimuna Salim:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na pia ninawashukuru vijana wetu ambao leo wameamua kututembelea katika Bunge hili Karibuni na tatu nimesimama kuunga mkono Hoja iliyoletwa na Mheshimiwa kwa niaba ya Mheshimiwa Madialo Mheshimiwa Mwenza Allen Katana (1GB).

Mimi nimesimama kuunga mkono kwa sababu huu Mswada tuko hapa sisi kwa kuweza kuwawakilisha wananchi wetu na hivi vitu ambavyo tunajaribu kuvizungumzia hapa na kuvipitisha ni vitu ambavyo tunavitegemea *immediately* vikifika kule kwa *executive* viweze kuchukuliwa kipao mbele kwa sababu kama wakati huu sasa hizi wa mvua, wakati wa nyuma tulikuweko tuna zile *pump* za kuweza kuvuta maji. Hata mimi kuanzia asubuhi ilikuwa napata simu kuna mahali kuna mafuriko, kuna shida nyingi ambazo zinahitaji hivi vifaa viweze kununuliwa na sisi kama Wabunge yatakikaniwa tukizungumza hivi tukipitisha ikija kwa budget tukipitisha tuone vitu vinafanyika kwa sababu wananchi wetu waliotuchagua ndio wanaumia.

Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono kwa sababu, saa hizi huu wakati ni mgumu, mashimo yameziba yanahitaji vitu vya ku *pump* maji, mabarabara ya *access* yana mashimo mengi, sisi ambao tunatoka huko Shanzu, wenye kutoka Nyali barabara ya Bombolulu tunaiona vile ilivyo na lau *it is a national* lakini kulingana na sheria kukiwa na *disaster* kama hivi tunahitaji kuwe kuna watu wetu wa Kaunti wanaweza kusaidia. Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu uweze kupita na tuhakikishe ya kwamba ukipita, tumeweka kwa bajeti na baada ya kuweka kwa bajeti tuhakikishe ya kwamba vifaa vimenunulia, watu wetu waweze kuishi buheri wa afya kuje mvua, kuje jua maisha yao yawe mazuri. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): When the Majority Leader is up standing then he is given precedence... So yes, Leader of Majority please make your contribution.

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I have heard the Motion, the spirit of the Motion in no doubt is a good one but this being a House of rules and procedure I doubt if the Motion made the threshold for it to be debated. Mr. Speaker if we go to section one of the County Government Act, subsection 1(1) it gives us the powers, the title of the section says, 'procedure for the exercise of legislative'. So, the power to legislate is directed in section (21) of the County government and the section says that, 'the County Assembly power shall exercise its legislative power through legislative first by the County Assembly and assented by the Governor. Mr. Speaker legislative entails Motion and Bills those are what we pass as an Assembly to instruct the executive to implement Mr. Speaker. Mr. Speaker sub section 4 of the same section 21 of the County Government Act states that, 'for the purposes of this Act, money legislative means that legislative contains provision dealing with the following...

[Silence]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Please proceed Honourable Mwamwiri.

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Sub section 4 Mr. Speaker I may repeat to read because we were in consultation that says "for the purposes of this Act money legislative means a legislative that contains provision dealing with taxes, deposition of charges on public funds or the variation or repeal or any of those charges (c) which is my concern Mr. Speaker, the appropriation on receipt. Mr. Speaker, the prayers of that Motion, detect that the department appropriates when it comes to appropriates that automatic goes to money legislative. If you go back to Standing Order 204 Mr. Speaker and I guess you have one with you there, entails for a Motion or legislative, it has to come through the Committee on Finance in consultation with the Finance Department. Mr. Speaker because of that I doubt if this Motion even if it will pass, going by those procedures, if it will be legit and the executive will be mandated to implement since it does not come from the Committee on Finance in consultation

with the Department of Finance. Therefore Mr. Speaker this being the House of rules and procedure I urge our Members, it is a good Motion but to follow the right procedure to direct to the Committee on Finance so that the Committee can consult with the department before it has been brought to this House for passing. So maybe the mover of the Motion Mr. Speaker, if he will be so pleased to withdraw the Motion or if he insist, I can guarantee because the other wing of the government are also informed, this Motion will not see the light of the day from that end. Thank you, Mr. Speaker I oppose.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Athman, according to our Standing orders 204 the first word there is, 'If' in the opinion of the Honourable Speaker and I am the Speaker, it is not in my opinion. Therefore, the debate as far as this Motion is concerned shall proceed, you have your right to vote otherwise, so the debate continues. Yes, Honourable Maryam Baimu?

*[Applause]*

**Hon. Baimu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote kuona siku ya leo, tukaamka salama salmini tukaweza kufika kwa Bunge letu. Pili, ningependa kuwakaribisha vijana wetu waliokuja Bungeni leo kuweza kusikiza ni mambo gani ambayo tunaweza kujadiliana hapa muweze kusoma kitu kimoja ama viwili. Karibuni sana, tatu mimi nimesimama Mheshimiwa Spika kuweza kuunga mkono hii Hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Allen Katana kwa sababu tukiangalia kusema ukweli katika Kaunti yetu tuko na upungufu wa hizi *grader* ama hizi mashine za kuweza kusaidia kule nyanjani katika barabara zetu katika *drainage* zetu. Mimi nikiongelea kidogo Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Allen Katana hapa amesema kwamba amepata usaidizi wa saruji malori kadha kule Bamburi Portland.

Mimi pia ni vile vile nimepata hizo saruji na shida ni ile ile ameongelea kwamba huko *transport* tukiulizia malori tunaambiwa ni mabovu; kwa hivyo kwa sasa hizo lori zangu za saruji bado zimekaa huko Bamburi nahangaika nitafute pesa niweze kukodisha lori, nahangaika nitafute pesa nitafute hiyo mashine niweze kulipia pale Portland, ili ile saruji iweze kuchotwa niingize kwa ile lori ambayo itakuwa nimekodisha ndio nipeleke kwa wananchi wangu wa Free Town. Kwa hivyo kusema ule ukweli Mheshimiwa Spika ni jambo la kusikitisha na hii hoja imekuja kwa wakati mzuri sana ikiwa tutaungana mikono Waheshimiwa Wenza, tuweze kupitisha hii Hoja na ikifika kule kwa *executive* iweze pia kuchukuliwa mstari wa mbele ama kipao mbele iweze kutekelezwa hizi lori ziweze kununuliwa kama ni hizi *grader* ziweze kununuliwa kwa sababu sote tunaamini kitu kimoja kukodisha hizi mashine ni ghali. Kwa hivyo ikiwa tutaweza kuweka *allocation* ziweze kununuliwa ziwe ni mali ya Serikali ya Kaunti nina imani sote katika Wadi zetu tutaweza kusaidia ikiwa mtu ako na shida kwa Wadi yake amepata pengine kama hizo saruji Bamburi Portland, unaweza kupata lori mara moja, unaweza kupata hiyo mashine ili uweze kuchota zile saruji ukajisaidia kwa Wadi yako. Kwa hivyo mimi nimesimama hapa leo Mheshimiwa Spika kuunga mkono shukran.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Maryam Baimu. Yes, Honourable Leila Mughazo Nyache, Member of the County Assembly (MCA) Kipevu please make your contribution.

**Hon. Nyache:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kuniona. Kwanza nachukua fursa hii kuomba msamaha wa kuchelewa Mheshimiwa Spika. Pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo, nyengine nakuomba Mheshimiwa Spika niweze

kuwakaribisha vijana wangu pale, wale baadhi yao wanatoka Wadi ya Kipevu na nimeona sura ambazo nazifahamu na nimemuona Patrick pale na wenzake. Kwa hivyo karibuni sana vijana wetu muweze kuona yale ambayo tunayo pambana nayo hapa Bungeni ama vile tunavyo wawakilisha watu wetu katika Bunge la Mombasa. Mheshimiwa Spika nimesimama pia kuunga mkono Hoja hii iliyokuja na Mheshimiwa mwenza ambaye ni Allen Katana, kwa kweli ni Hoja mzuri sana na Hoja hii kulingana na hizi changamoto ambazo ziko hapa katika hiyo Hoja ya kwamba vifaa hakuna katika *Department ya Transport* vifaa kadha kama hivyo wenzangu walivyotaja kama vile magari, ma *loader* na kadhalika. Inagusa Wadi zote sio Wadi moja, ni Wadi zote zinaguswa za Mombasa kulingana na sasa hivi hii mvua inanyesha kuna barabara ambazo hazijajengwa vizuri, kuna barabara hazijaingiliwa kuna mahali kuna mashimo, maji yanasimama pale hatujui hata tutafanya nini? Cha msingi hapa ni kuundwe ile *disaster committee* na wakati wa nyuma, ilikuwa ile Kamati ya *disaster* lakini sasa hivi hatuioni na hata sijui iko wapi? wala haifanyi kazi sijui ilikuweco tu ni mfano ama ni vipi? Hiyo *disaster committee* ni muhimu sana Mheshimiwa Spika, iweze kuingilia kati masuala haya ya kuwa waweze kuangalia mafuriko yako wapi, ni wapi kumesimama maji...

[*Interruption*]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Leila hii Kamati ya *disaster* unazungumzia wasema iundwe, iundwe wapi? Kijijini kwako? Kwa Bunge? Mawaziri? Wataka iundwe wapi?

**Hon. Nyache:** Iundwe Kaunti nzima ya Mombasa kwa sababu...

[*Interruption*]

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Leila kile tunafaa kuelewa ni hii Kamati unayosema iundwe ya *disaster* inaundwa wapi? Kwa Bunge la Mombasa ama katika upande wa executive ambayo inaongozwa na Gavana?

**Hon. Nyache:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunieleweshwa, iundwe kwa upande wa executive, tuko pamoja na kwa kila Wadi kuwe na hizo Kamati ambazo zitaweza kusaidia.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Mwamwiri...

[*The Leader of Majority Party Honourable Athman Mwamwiri off microphone*]

Please be on record.

**The Leader of Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker I wish to inform the House that the said Committee on Disaster is already in place and the Chair is the CEC for Public Administration Honourable Ambani and also sub-county level Honourable Speaker, the Committees are also there. It is unfortunate that the representations are not from the Assembly but the Ward Administration are part of the Committees at the Sub-County Level Mr. Speaker. Thank you, Mr. Speaker, so Honourable Member be assured that the Committees are there are, maybe the issue is that the Committees is to be established, the Committees are there Mr. Speaker. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, Honourable Leila Nyache, I hope you are well guided and informed, now continue.

**Hon. Nyache:** Ahsante Mheshimiwa Spika na ahsante Kiongozi wa Wengi kwa kuweza kumwelekeza mama yako, lakini mimi nimesikia wenzangu wote wakilalamika inamaanisha hiyo Kamati haijaanza kufanya kazi. Kwa hivyo ningeomba hiyo Kamati ianze kazi mapema, kwa sababu ya hizi shida watu wanazopata za hizo magari hakuna na hizo *loaders* hakuna mara unaambiwa magari yameharibika mara nini mambo ni mengi. Mimi kwanza niruhusu kidogo niingililie upande wa Mazingira Mheshimiwa Spika upande wa Mazingira tafadhali magari ni machache...

*[Applause]*

Magari ni machache upande wa Idara ya Mazingira...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Leila...

*[Interruption]*

**Hon. Nyache:** Mheshimiwa Spika ni ruhusu tu...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Mheshimiwa Leila unaruhusiwa na Kanuni za Bunge hili kuleta hoja kama hiyo ya masuala ya Mazingira.

**Hon. Nyache:** Sawa wacha nijalize kabisa kwa sababu ni....

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): ...kulingana na Kanuni za hili Bunge, kwa sababu hata yale ambayo utayasema hayawezi tekelezwa endapo hoja ambayo iko mbele yetu inahusiana na Idara tofauti...

*[Interruption]*

**Hon. Nyache:** Sawa.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): ...Kwa hivyo yale ambayo unataka kusema na yale ambayo yamejaza moyo wako ni mawazo mazuri lakini ukitoka hapa enda tengeneza hoja inayohusiana na Idara husika ulete itazungumziwa.

**Hon. Nyache:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa hivyo mimi nasema ya kwamba magari hakuna ya matakataka, taka zimejaa katika Mombasa yetu...

*[Applause]*

Na Mheshimiwa Spika utanisamehe kwa hilo. Ahsante sana.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, Honourable Ibrahim Omondi Oyugi please make your contribution.

**Hon. Omondi:** Thank you Mr. Speaker Sir for the opportunity that you have given me...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Omondi...

---

*[Interruption]*

**Hon. Omondi:** Yes.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Omondi...

**Hon. Omondi:** Yes, Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Sergeant at Arms, please confirm whether Honourable Omondi is well dressed to be in the Plenary.

*[Interruption]*

**Hon. Omondi:** Honourable Speaker is always blind, Mr. Speaker. I do not know whether you are within the Standing Orders of this Honourable House? The Speaker should remain blind, Mr. Speaker. I wonder that today you are able to see Mr. Speaker, what is happening?

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Athman Mwamwiri what are you saying?

**The Leader of the Majority Party** (Hon. Mwamwiri): Mr. Speaker the Member I doubt if he is aware that he was coming for a Plenary session Mr. Speaker because the way he is dressing Mr. Speaker you cannot differentiate with Mungiki Mr. Speaker...

*[Laughter]*

So, I urge Mr. Speaker to ask Sergeant at Arms to confirm if the Member is properly dressed.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, please Sergeant at Arms because this is a House of Rules, Procedures and Records please confirm the grooming status of Honourable Omondi to just confirm whether he is fit to be in the Plenary meanwhile Honourable Manuari please make your contribution as the Sergeant at Arms do their work.

**Hon. Juma Manuari:** Ahsante Mheshimiwa Spika nichukue fursa hii kwanza kumshukuru...

*[Laughter]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Manuari...

*[Interruption]*

**Hon. Juma Manuari:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Yes, Honourable Members, as earlier stated we have our Standing Orders that guide us on our way of how we should groom ourselves as we come to the Assembly. Maybe Honourable Ibrahim Oyugi was rushing to come to the Plenary to attend this important business. However, we will allow the Sergeant at Arms to help him do the right grooming then he comes back to the Plenary. Thank you.

*[Applause]*

Honourable Manuari?

**Hon. Juma Manuari:** Ahsante Mheshimiwa Spika nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nichukue fursa hii kuwakaribisha vijana wenzangu katika Bunge la Mombasa na hapa ndipo tunapofanya yale mambo yetu na kuhakikisha kule mitaani mwenu mambo yanakuwa sawa. Mimi Mheshimiwa Spika kutokana na Hoja ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana, *I GB* rafiki yangu wa kudumu nimesimama kuunga mkono...

*[Applause]*

...na kutokana na wakati na muda sitaki kusema sana kwa sababu hiyo yenyewe ripoti yake tayari ishajieleza. Kwa hayo Mheshimiwa Spika nauunga mkono. Ahsante sana.

**The Temporary Speaker (Hon. Makanga):** Thank you. Yes, Honourable Pamela Ojala please make your contribution.

**Hon. Ojala:** Thank you Mr. Speaker for the opportunity. I want to thank the Almighty God Mr. Speaker for giving us this golden opportunity today; again, I want to acknowledge the presence of our good Gen Z's in this Honourable House, feel welcome this is a House of debate and records I hope you came here to learn this morning. Mr. Speaker as I embark on the discussion, I rise to support the Motion as my colleague Honourable Member of Bofu Ward has stated that the Motion is well elaborated and speaks for itself Mr. Speaker. Mr. Speaker, I will not have much time to dwell on the Motion, and I thank also the Majority Leader to inform the House that we have the Committee on Disasters the Committee will be able to help us in the prevention, the good mitigation, the recovery and the response. Mr. Speaker, I stand to support the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker (Hon. Makanga):** Thank you so much, Honourable Pamela. Yes, Honourable Shuhudia Abdallah please make your contribution.

**Hon. Shuhudia Abdallah:** Ahsante Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono. Ahsante.

*[Applause]*

**The Temporary Speaker (Hon. Makanga):** Honourable Nusura Mwinyi Kimuswa?

**Hon. Nusura Mwinyi:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niwatambue wageni wetu waliokuja hapa kuja kutizama wale viongozi walio wachagua zile shughuli wanazozifanya. La pili, nataka nimpongeze Mheshimiwa mwenza, Bwana Allen Katana, *IGB*...

*[Applause]*

**The Temporary Speaker (Hon. Makanga):** Honourable Nusura, we do not have such a Member in this House, please confirm to get the right name for record purposes.

**Hon. Nusura Mwinyi:** Ahsante kwa kunirekebisha, Mheshimiwa Allen Katana kwa kuleta hoja hii nzuri ambayo itatuletea natija katika jamii zetu. Kwanza nataka niseme katika msimu huu tulio nao sasa wa mvua, tumeona majanga mengi kwanza nimetumia jumbe nyingi sana nikiwa papa hapa kumefurika, kuna matakataka mengi ambayo yameziba mashimo ambayo yanafanya maji hayaendi; kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kuunga mkono hii hoja nzuri iliyoletwa na Mheshimiwa Allen Katana ni hoja ambayo itatuletea natija. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you so much Honourable Nusura. Yes, Honourable Juma Kambi please make your contribution, Chairperson Environment and *takataka*, is that what you said?! Chairperson, Environment and Waste Management please make your contribution.

**Hon. Juma Kambi:** Mheshimiwa Spika kabla niongee mwambie...

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Juma Kambi you are out of order first. You cannot address the Honourable Speaker while seated.

**Hon. Juma Kambi:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu na pia vile vile huu Mswada umekuja kwa wakati mwafaka kwa sababu saa hii kila mahali ni maji, kila mahali ni maji, maji...na yote ni kwa sababu tu ya hali duni ya barabara zetu. Kwa hivyo tunaomba Jumba hili na pia vile vile huu Mswada uweze kutekelezwa kwa haraka kwa sababu sote tulioko hapa hakuna hata mtu mmoja ambaye hajatukanwa, hajapigiwa kelele katika mitandao kwa sababu ya maji katika barabara zetu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika lakini kabla nikae tafadhali Kiongozi wa wengi asimame aniombe msamaha ndio nikae. La sivyo nitasimama vivi hivi mpaka Bunge livunjwe hapa.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable...

*[Interruption]*

**Hon. Juma Kambi:** Wewe waweza....

*[Interruption]*

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Honourable Juma Kambi you are out of Order! This is not a market place. So, take your seat. Honourable Allen Katana please reply to the Motion.

*[Consultations]*

Honourable Juma Kambi you are out of Order please!

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika nikushukuru kwanza kwa hekima yako ya kadiri unavyo liongoza Bunge hii asubuhi ya leo. Pili Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mungu kwa kunipa viongozi kama hawa ili kuweza kufanya nao kazi kwa sababu pia nimeona nia ya mioyo yao ni ya kuhudumikia watu wetu walio tuweka katika nyadhifa hii na kwa kuwa nimekaa hapa na Kiongozi wa Wengi na ana tajiriba kwa lugha ya Kiswahili atanieleza maana ya *summary* kwa ufupi kwa mukhtasari Mheshimiwa Spika nitataja mawili matatu ambayo yalikuwa tu ndio maombi ya swala hili; ya kwamba sisi tulitaka tu katika mipangilio yao hao *Executive* wawe wataweka maoni haya yetu katika mipangilio yao kwa sababu sisi kama wawakilishi wa wananchi kule mashinani ndio fikra tunazipata moja kwa moja shida za watu wetu hawa na tena kipengele cha pili kikawa kinasema ni vizuri vitu hivi vitakapo patikana, magari haya yatakapo patikana yawe yanaweka kimpangilio isisemekane peke yake ni Kisauni ndio wanaomiliki ama ni Mvita pekee yake ndio wanaomiliki kuwe na ratiba na ile itifaki ya jinsi itakavyokuwa itafanya kazi iweze kufwatiliwa Mheshimiwa Spika, na tena utaniruhusu hili nilitoe kama mfano siku mbili zilizopitia tulikuwa na Mstahiki Gavana katika hospitali yetu kubwa ya Utange pale Shanzu na tukagundua tumekuwa kwa muda mrefu tuna giza na mkandarasi aliyepewa kazi pale Mheshimiwa Spika baadhi ya zile kazi alikuwa amepewa ni

kuleta *generator* ambayo kwa Kiswahili sijasomea hapo, na kwa hakika *generator* ya ghali sana ililetwa lakini hii generator tokea iletwe ni miezi sita Mheshimiwa Spika na *generator* haijawahi kufanyiwa *service* na hivi sasa ninavyosema *generator* ile imeharibika. Ndipo sasa ikawa ombi ya aliyeleta Mswada huu, katika ombi lake la tatu, ni kwamba zitakavyo letwa *mashine* hizi ama magari haya kuwe na mpangilio hususan wa ambapo tarehe ikifika ziwe zinafanyiwa huduma ili ziendeleo kutuhudumia kwa muda mrefu. Mheshimiwa Spika nikikaa nataka nitangaze rasmi ya kwamba Mheshimiwa Nusura hajafanya makosa kuniita *IGB* maana jina hilo lilifwata ratiba inayostahiki nikapewa gazeti na gazeti hilo liko kwa mikono kwa *Human Resource* wetu; kwa hivyo Mheshimiwa Spika wana ruhusa ya kuniita *IGB*, ahsante.

**The Temporary Speaker** (Hon. Makanga): Thank you Honourable Allen Katana and for avoidance of doubt, maybe that communication needs to reach my seat so that we are able to address you as such. However, from our records you remain to be referred to as Honourable Allen Katana, Honourable Allen Rogers Katana. Honourable Members, having debated the Motion by Honourable Allen Katana, the Motion on Budgetary Allocation for Road Maintenance Machinery to Enhance Service Delivery by Honourable Jactone Madialo, brought to the House on his behalf by Honourable Allen Katana duly debated by this Honourable House, I now put the question that the said Motion be adopted.

*[Question put and agreed to]*

The Motion is adopted. Yes, Clerk?

### ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday 6<sup>th</sup> May, 2025 at 2:30p.m. Thank you, enjoy your lunch.

The House rose at 1:30p.m.